



Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222
Faksi: +255 22 2111281
B/Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Machi 31, 2015

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kulaani tukio la kuuwawa kwa Askari Polisi na kujeruhiwa kwa Wanachama wa CUF

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kuuwawa kwa askari polisi wawili waliokuwa kazini na kuibiwa silaha, tukio lililotokea usiku wa Machi 30, 2015 huko Kongowe, Wilayani Temeke, jijini Dar es Salaam.

Kutokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 14, kila mtu anayo Haki ya Kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria. Hivyo, kuuwawa kwa askari polisi ambao ni walinzi wa usalama na amani, tena wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao ni kitendo kinachopaswa kulaaniwa vikali na kila mwananchi.

Pia Tume imesikitishwa na tukio la hivi karibuni la kuvamiwa, kupigwa na kujeruhiwa kwa wafuasi takriban 25 wa Chama cha Wananchi (CUF) waliokuwa wakitoka mkutanoni Makunduchi, Wilaya ya Kusini Unguja, tarehe Machi 29, 2015.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inalaani matukio hayo yote kwa kuwa yanaenda kinyume na haki za binadamu.

Aidha, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara ya 18 (a) inasema kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake, na ibara ya 20 (1) inaeleza kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine, na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.


Pia kutokana na Sheria ya Vyama vya Siasa Sura 258 ya mwaka 2002, ibara ya 11 (1)(a) kila chama cha siasa kilichopata usajili wa muda au kudumu kina haki ya kufanya mikutano ya hadhara katika maeneo yoyote ya Jamhuri ya Muungano

baada ya kutoa taarifa kwa Mkuu wa Polisi katika maeneo husika kwa nia ya kujitangaza na kutafuta wanachama, 11 (1)(b) kulindwa na kusaidiwa ulinzi kwa ajili ya kuleta amani na utulivu katika mikutano hiyo.

Tume inawataka wananchi kuheshimu haki za binadamu na kuwa na uvumilivu wa kisiasa hususan kipindi hiki nchi yetu inapokabiliwa na matukio makubwa ya kupigia kura ya maoni ya Katiba Inayopendekezwa na uchaguzi mkuu, hapo mwezi Oktoba.

Pia Tume inawaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi la Polisi katika kuhakikisha watu waliofanya matukio hayo wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo husika ili sheria ichukue mkondo wake.

Imetolewa na:



Mhe. Bahame Tom Nyanduga
Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Machi 31, 2015